



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.MZA/KDC/S.10/40/41

21 Aprili, 2022

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba amepokea Kibali cha Ajira Mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia Barua yenye Kumb.Na.FA.170/359/01"B"/47 ya tarehe 15 Machi, 2022.

Hivyo anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa za kujaza nafasi zifuatazo:

1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III – NAFASI NNE (4)

1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Waombaji wanatakiwa awe mwenye Elimu ya Kidato cha Nne (Form IV) au Sita (Form Six) aliyehitimu astashahada/cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

1.2 MAJUKUMU

- I. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- II. Kusimamia mapato na matumizi ya Serikali ya Kijiji.
- III. Kusimamia ulinzi na usalama wa Raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- IV. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya maendeleo ya Kijiji.
- V. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- VI. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- VII. Kuandaa Taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha Wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- VIII. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.
- IX. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.

Uk. 1

1.3 MSHAHARA

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali yaani TGS B.

1.4 MASHARTI YA JUMLA

- I. Waombaji wawe ni Raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18 hadi 45.
- II. Waombaji wawasilishe maelezo binafsi (Curriculum Vitae) yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye Anuani na Namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.
- III. Waombaji wawasilishe picha ndogo mbili za hivi karibuni (passport size).
- IV. Waombaji waambatanishe nakala za vyeti vya Kidato cha Nne au Sita, Taaluma na cheti cha kuzaliwa. Waombaji watakaowasilisha "Result Slip", "Statement of Results", "Provisional Results" au "Transcripts" **HAVITAKUBALIKA.**
- V. Kwa Waombaji waliosoma nje ya Nchi Elimu ya Kidato cha Nne au Sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).
- VI. Kwa waombaji waliosoma Vyuo nje ya Nchi wawasilishe uthibitisho kutoka NACTE.
- VII. Waombaji watakokidhi sifa zinazotakiwa ndio watakaoitwa katika usaili.
- VIII. Waombaji waandike namba ya Kitambulisho cha Taifa katika barua zao za maombi ya kazi au waambatanishe nakala ya Kitambulisho cha Taifa kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
- IX. Barua ya maombi iliyosainiwa na Mwombaji inawezakuandikwa kwa lugha ya Kiingereza au Kiswahili.
- X. Waombaji wenye mahitaji maalum (special needs/disability) wanatakiwa kuainisha kwenye maombi yao.
- XI. Waombaji watakaowasilisha Taarifa za kughushi watachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria za Nchi.
- XII. **Maombi yatakayoletwa moja kwa moja bila kupitia Posta hayatafanyiwa kazi.**
- XIII. **Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 05 Mei, 2022 saa 9:30 Alasiri. Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta kwa Anuani ifuatayo:**

**Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya.
S.L.P. 88,
NGUDU-KWIMBA.**

Tangazo hili pia linapatikana katika tovoti ya Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba
www.kwimbadc.go.tz

Tangazo hili limetolewa na;

H.J. Msanga,
**MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA KWIMBA.**

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA KWIMBA**

Uk. 2